# Kiongozi asiyewajibika...

# Tufanyeje?



Kijitabu hiki kimetayarishwa na watendaji wa Twaweza Tanzania wakishirikiana na viongozi wa dini.

Mwandishi: Evarist Kamwaga
Mchoraji: Marco Tibasima
Mhariri: Rakesh Rajani

©Hivos/Twaweza 2010

SLP 38342, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 266 4301
Faksi: +255 22 266 4308
Barua pepe: info@twaweza.org
Tovuti: www.twaweza.org

Unaruhusiwa kunakili sehemu yeyote ya kijitabu hiki kwa sababu zisizo za kibiashara tu. Unachotakiwa kufanya ni kunakili chanzo cha sehemu uliyonakilia na kutuma nakala mbili kwa Twaweza.

# Utangulizi

Ndugu msomaji:

Hebu fumba macho kidogo. Ungependa maisha yako yaweje? Vipi kuhusu maisha ya familia, jirani, rafiki? Hali ya uchumi au kipato chenu iweje? Ubora wa elimu? Upatikanaji wa huduma za afya? Maji safi? Urahisi wa na gharama za mawasiliano? Hali ya usalama? Unafikiri umekwishafikia hatua uliyostahili kimaisha?

Ni nani anawajibika kutimiza ndoto zako?

Mara nyingi tunategemea viongozi kutuletea mabadiliko na maisha bora. Ni kweli viongozi wana wajibu wa kuwezesha maendeleo. Lakini tukiwaachia pekee yao, viongozi watashindwa. Viongozi wanatuhitaji sisi kutumia akili na busara tulizopewa na Mwenyezi Mungu kuwachagua wale wanatuofaa. Na baadaye kuwasaidia, kuwashauri na kuwawajibisha.

Kwa sababu kiongozi aliyechaguliwa nasi anapaswa awe *mtumishi wa watu,* anayetumikia jamii. Siyo bosi, siyo Bwana Mkubwa, siyo mtu anayetumia vitisho au kuwaendesha wananachi. Tukiwa makini, kiongozi pia atakuwa makini. Tukisinzia au kukubali kudanganywa, basi na yeye atajua ameachiwa nafasi ya kufanya vyovyote anavyotaka.


Kijitabu hiki cha hadithi kimetungwa kusisimua fikra na hatua makini wakati huu wa uchaguzi na baada yake . Maudhui yake yametokana na *Tamko la Pamoja la Viongozi wa Dini wa Kiislamu na Kikristo kuhusu Uchaguzi Mkuu 2010* (rejea ukurasa 23) lililotolewa

hadharani. Tamko hili linaelezea pia sifa za mgombea na viongozi wanaofaa. Tunawashukuru viongozi hawa kututungia mwongozo uliojaa nasaha, busara na udhihirisho wa mapenzi mema kwa nchi yetu.

Basi ni juu yako sasa kuamua na kuchukua hatua. Uwezo wa kutimiza ndoto na shauku yako uko mikononi mwako. Chagua wawakilishi wako vizuri, kisha wasaidie na wawajibishe wafanye kazi zao.

*Pamoja twaweza. Ni sisi!*

Rakesh Rajani
Mkuu, Twaweza


WAHUSIKA
Ni wanasiasa wanaotafuta kura za wananchi.
Mzee Fundi, Kala chumvi nyingi na pia ameona mengi, mume wa Amina.
Bonge, Kijana mjasiriamali na mchambuzi wa mambo.
Amina, mkulima mchapakazi, mke wa Mzee Fundi.


Utafiti unaonyesha kuwa robo tatu ya wanafunzi nchini wanafeli hisabati!


Elimu inazidi kudorora, wanasoma hadi sekondari lakini hawawezi kusoma wala kuhesabu!
Inachanganya, majengo mazuri, wahitimu `bomu' kabisa!


Nadhani baada ya uchaguzi viongozi watazi-fanyia kazi kero zote hizi.
Mke wangu, achana na porojo za wanasiasa, wanatudanganyadanganya na kututumia, baadaye `bai bai'!


Afya ndio usiseme... Serikali imejitahidi sana kujenga zahanati lakini huduma mbooru!
Kweli. Hata maji ni tatizo, huoni visima vyote vitatu vimekufa!
Na wanaoumia zaidi ni wanyonge kama yule jirani yetu mjane na hata yatima.


Mvi zote hizi kichwani, tumeona mengi. Tangu kabla ya uhuru, nimewachambuaaa, hakuna lolote... wanasiasa ni maneno na kula tu!


Mara ujumbe wa simu unaingia...
Nani tena huyu?
Aha! Kumbe kuna mkutano sokoni, mgombea anagawa pilau kuwashukuru wananchi.
Changamka twende!


Danganya toto hiyo. Ukichambua...
... Mume wangu, utakufa na huo uchambuzi wako... Twende zetu tukajizolee vya 'dezó'!
Haya basi twende tukapoteze muda, kwanza kura yenyewe sitopiga.
Hasama 2010


Sokoni...
Kama ninavyowaeleza siku zote...
...ni mimi pekee nitakayewaletea maendeleo..!
Au mmesahau?! Wakubwa wote wananifahamu.
PILAU!


Nikipiga simu moja tu... wanaitikia ndiyo mheshimiwa!
Kwa hiyo nitawalisha mema ya nchi hii. Au sio ndugu zangu?
Sijui khanga zipo?
Pilau lenyewe bado?
Vuta subira!


Mkinichagua mimi kwanza nitawaletea maji ya bomba kwa kila nyumba, chupa kubwa ya 'rangimbili' kwa kila mmoja. Pili, kila mtoto atapata elimu ya 'inglishi' na digrii juu! Pia barabara za lami kama ulaya...
...na kwa mwenyekiti hapa shangingi jipyaaa!
Makofi!
Makofi!
Makofi!


Eti wazee wangu...
Mimi mtoto wenu kabisaaaa,
kabila moja, dini moja....
lakini hao 'wakuja' tu...
Au sio jamani?
Asanteni!
Ndi yooooo!
Waambieee!
Oyeeeee!
Wataipatapata!


Kura zetu umepataa!
Aisee huyu mgombea 'bomba'!
Du! Sitougua tena miye, chupa za rangi mbili kila mtu?!
Jamani! Wanangu wakishajua 'inglishi' tu wataanza kujichotea ma-posho 'kedekede' kwenye ma-semina...


Sijui watanzania akili zetu zilirogwa?! Tunadanganyika kirahisi sana, tutaaminije ahadi kama hizi?
Halafu anatugawa huyu! Anatumia ukabila na udini kama tiketi ya kuchaguliwa!



Ahadi zitatekelezwa tu. Si anafahamiana na vigogo bwana! Halafu ni tajiri.
Hapa, hamna kitu! Wacha tule pilau kisha tukahangaikie maisha yetu tu...


Mzee fundi, sisi tukikata tamaa nani atatukomboa?
Tutalalamika wee, hali ngumu iko pale pale. Kumbuka, maji hayachemki kwa kuyatazama tu!


Mgombea mwingine...
Naomba kura zenu...
Siyo kwa sababu nina pesa za kuwaletea maendeleo, au kuwanunulia 'mizawadi'.
Anacheza huyu...
Du! Sasa huyu mgombea gani?!


Maendeleo yetu yataletwa na juhudi zetu wenyewe...
... Siyo utajiri au ruzuku 'Kibao' za serikali au misaada toka kwa wazungu...
Huyu hatotusaidia, hatufai kabisa!
Mh! Hakuna ahadi? Huyu mwanasiasa kweli?
Hayo maendeleo yatakujaje sasa?


Twaweza kufanya mengi...
Kuboresha elimu kwa kufuatilia utendaji wa walimu na ustadi wa kujifunza kwa watoto wetu...
...Kutovumilia vitendo vya rushwa, kudhibiti upotevu wa dawa mahospitalini, na kuhimiza matumizi sahihi ya dawa...
...Kuwa wabunifu katika kutatua kero zinazoikabili jamii yetu...
Na zaidi kuiwajibisha serikali kuu na za mitaa kiutendaji...
...Pia kujifunza toka kwa wengine, Asanteni!


Wanatafuta kura zetu leo...lakini je, watakuwa pamoja nasi kwa miaka mitano?
Kwani sisi tunahitaji kiongozi wa aina gani?


Awe mcha Mungu!
Anayejali na kuwastahi watu!
Anayependa haki na kuwajali wanyonge!
Awe anajua na kuitetea katiba ya nchi na azingatie sheria!
Awe mkweli kwa maneno na matendo!
Anayeshirikiana na wote bila ubaguzi!
Awe mwenye uwezo wa kuongoza na upeo mpana!
Awe mpenda amani na utulivu!
Awe mwadilifu!
Awe anayelipenda taifa lake!


Mungu ametupatia akili tufanye maamuzi ya busara hasa katika kuchagua viongozi bora
TAMBUA, uamuzi wako wa leo, si tu utaathiri maisha yako ya sasa bali na vizazi vijavyo...
Fanya chaguo makini... CHAGUA KWA BUSARA!

## TAMKO LA VIONGOZI WA DINI KUHUSU UCHAGUZI MKUU WA 2010

Sisi Viongozi wa Dini kutoka Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) na Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar tuliokutana hapa Dodoma tarehe 18 Augusti 2010 kutafakari juu ya Hali ya Amani ya nchi yetu hasa wakati wa Uchaguzi Mkuu.

**TUNATAMBUA KWAMBA** tarehe 31 Oktoba 2010 itakuwa siku ya kuwachagua viongozi wetu wa kisiasa yaani Madiwani, Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Rais wa Jamhuri Muungano wa Tanzania. Mchakato huu wa Uchaguzi Mkuu umekwishaanza kwa kuboresha Madaftari ya wapiga kura na Vyama vya Siasa kuteua wagombea wao katika nafasi hizo zitakazopigiwa kura. Kisha kutakuwa na uteuzi rasmi wa wagombea utakaofanywa na Tume ya Uchaguzi Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) zikifuatiwa na kampeni, kupiga kura na kutangazwa matokeo.

**TUNAWAPONGEZA** wale wote ambao wamefanikisha hatua za awali kwani hatua hizo zimefanyika kwa amani. Hata hivyo, tunahimiza kuwa dosari zilizojitokeza (tuhuma za utoaji rushwa na baadhi ya watu kutokubali matokeo na kuandamana) zitazamwe na kushughulikiwa ili zisije zikaleta migogoro yenye kuleta madhara ya kuteteresha amani na umoja wetu wa kitaifa wakati na baada ya mchakato wa uchaguzi.

Vile vile sisi viongozi wa Dini tunampongeza Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Viongozi wa vyama vya CCM na CUF huko Zanzibar (Mheshimiwa Rais Aman Abeid Aman Karume na Katibu mkuu Maalim Seif Sharif Hamad) kwa kufikia muafaka wa kisiasa. Kadhalika tunawapongeza wananchi wa Zanzibar kwa kufanya uamuzi wa kuridhia kuundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Tunaomba Serikali, Vyama vya Siasa na wadau wengine kuendelea kuelimisha wananchi juu ya aina hii ya serikali. Vile vile tunataka wale watakaohusika katika uundaji wa serikali hii mara baada ya Uchaguzi Mkuu, waiunde kwa dhati na uzalendo ili iweze kufanya kazi iliyotarajiwa ya kudumisha amani na kuleta maendeleo.

Pamoja na hayo, tunalishukuru Bunge letu la Jamhuri ya Muungano na Serikali yetu kwa kupitisha na kuweka Sheria ya Gharama za Uchaguzi. Matumizi ya fedha yasiyo halali kwa ajili ya kupata kura yalikuwa kero kwetu na mara nyingi yaliweka madarakani baadhi ya watu wasiokuwa na sifa za uongozi bali utajiri wao. Kinachotakiwa sasa ni kuitekeleza na kuisimamia kikamilifu sheria hii. Hata hivyo, sheria hii haijafahamika kwa wananchi wa kawaida. Hivyo itolewe elimu ya kutosha juu ya sheria hii ili kutoa mchango mkubwa katika ufanisi na utekelezaji wake.

**TUNAWAOMBA** wale wote waliojiandikisha kufuatilia kampeni za uchaguzi za wagombea wa vyama vyao vya kisiasa ili wafahamu sera na mipango ya wale watakaoifanya kama wataingia madarakani. Ikifika siku ya kupiga kura waende kupiga kura wakijua kwanini

wanampigia mgombea huyo au chama hicho cha kisiasa. Wakati wa kupiga kura, tumpigie mgombea mwenye sifa zifuatazo:

- Awe mcha Mungu
- Anayewajali na kuwastahi watu
- Anayependa haki na kuwajali wanyonge
- Awe anaijua na kuitetea Katiba ya nchi
- Awe mkweli kwa maneno na matendo
- Anayeshirikiana na wote bila ubaguzi
- Awe mwenye uwezo wa kuongoza na upeo mpana
- Awe mpenda amani na utulivu
- Awe mwadilifu
- Awe na moyo wa uzalendo yaani anayelipenda taifa lake

**TUNAWATAHADHARISHA** wananchi kuwa uamuzi wa kuchagua chama au mgombea usivutwe na rushwa, udini, kabila au sehemu anayotoka. Vyama vya Siasa au mgombea visijaribu/asijaribu kutumia hayo katika kuvutia wapiga kura. Viongozi wa Dini kushabikia waziwazi Chama cha Siasa au mgombea ni hatari. Atawagawa waamini kitu ambacho kinaweza kuleta vurugu na mgawanyiko katika eneo husika na pia kitaifa. Viongozi wa Dini wasiruhusu nyumba au sehemu za Ibada kutumika kwa ajili ya mambo ya kisiasa.

Matumizi ya Vyombo vya Habari kwa manufaa ya kibinafsi ni hatari kwa taifa letu. Vyombo hivyo vizingatie maadili mema pasipo kupotosha habari. Habari zisizo na ukweli zinaweza kuchochea chuki na vurugu.

**TUNATOA WITO** kwa Vyama vya Kisiasa, Wagombea, na vyombo vyote vinavyohusika katika uchaguzi mkuu zikiwemo serikali zote mbili zihakikishe kwamba uchaguzi unakuwa huru na wa haki. Hii itawezekana tu endapo maadili ya uchaguzi yanazingatiwa na kutekelezwa kwa hiyo tunawaasa toeni ahadi zinazotekelezeka. Epukeni jazba, kampeni za kashfa na vurugu. Hii itawapa fursa wapiga kura kufanya uamuzi bila woga na ulio sahihi kwa manufaa ya nchi.

Pia itawapa nafasi vyombo vinavyosimamia uchaguzi kusimamia kwa makini zaidi. Kama taratibu zitafuatwa basi matokeo ya uchaguzi yataonyesha matakwa ya wananchi na kukubalika na wadau wote. Ikiwa kutakuwa na dosari yoyote basi taratibu zilizowekwa zitumike na sio vurugu.

Ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na amani wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu:

- Viongozi wa Dini tutajitahidi kukutana na Viongozi wa Vyama vya Siasa ili kutoa rai yetu na kuwakumbusha wajibu wao wa kuhakikisha kuwa taratibu zote zinafuatwa na pale kutakapokuwa na jambo linalotishia amani juhudi za makusudi zitumike ili kulikabili na kuweka mambo sawa.
- Tutawaelimisha na kuwahamasisha wapiga kura kuhudhuria kampeni, kupiga kura na pasipo kushabikia vurugu wakati wote wa mchakato wa uchaguzi na baada ya uchaguzi.
- Tunawahimiza waumini wa dini zote kuombea uchaguzi wenye Amani.

Msomaji: Baada ya kusoma kijitabu hiki una fikra gani? Usibaki kimya. Jadili na wenzio. Tafakari pamoja na kiongozi wako wa dini. Kisha, chukua hatua kuhakikisha uongozi bora.

Pia unaweza kutuma maoni yako kwa vyombo vya habari. Anwani ya baadhi ya vyombo hivyo zinapatikana hapa.

| **Chombo cha habari** | **Namba ya Faksi** | **Simu ya mezani** | **Barua pepe** | **Simu ya Mkononi** | **Sanduku la Posta** |
|---|---|---|---|---|---|
| Majira | 022-2150987 | 022-2118377/9 | majira2006@btl.co.tz | 0754-314875 | 71439 DSM |
| Mtanzania | 022-2460030 | 022-2461459 | mtanzania95@hotmail.com | 0754-303552 | 4793 DSM |
| Mwananchi | 022-2450881; 2450886; 2450873 | 022-2450875/8 | mwananchipapers@ mwananchi.co.tz | 0754-780647 | 19754 DSM |
| Nipashe | 022-2700146 | 022-2700735/7 | mhariri@nipashe.co.tz | 0784-333186 | 31042 DMS |
| Tanzania Daima | 022-2126234 | 022-2126232 | tzdaima@freemedia.co.tz | 0754-001010 | 15261 DSM |
| Uhuru | 022-2183780 | 022-2180544 | uhurunews@yahoo.com | | 9221 DSM |
| Rai | 022-2460030; 2123186 | 022-2461459 | raihcl@yahoo.com | 0754-303552 | 4793 DSM |
| Clouds FM | 022-2124649 | 022-2118378/9 | cloudsfm@clouds.com | | 31513 DSM |
| ITV/Radio One | 022-2775915 | 022-2775916 | itv@ipp.co.tz | | 31042 DSM |
| TBC1 | 022-2866383 | 022-2860760 | tvt-dg@africaonline.co.tz | | 31519 DSM |
| Raia Mwema | 022-2401311 | 022-2401310 | info@raiamwema.co.tz | 0784-263871 | 11079 DSM |
| Mwanahalisi | 022-2760560 | 022-2760560 | halihalisi06@yahoo.com | 0784-440073 | 67311 DSM |


Mungu ametupatia akili tufanye maamuzi ya busara hasa katika kuchagua viongozi bora
TAMBUA, uamuzi wako wa leo, si tu utaathiri maisha yako ya sasa bali na vizazi vijavyo...
Fanya chaguo makini... CHAGUA KWA BUSARA!